HAKIARDHI

TUZO YA UANDISHI WA KIUCHUNGUZI KWENYE MASUALA YA NISHATI UOTO ILIYOTOLEWA KWA WAANDISHI 3 TEREHE 16 NOVEMBA 2011

USULI

- Kumekuwa na hitaji la kufanya uandishi wa kiuchunguzi katika maeneo mbalimbali ili kuibua masuala yanayoigusa jamii ya wazalishaji wadogo.
- Umuhimu huo unatokana na ukweli kuwa, yapo masuala mengi muhimu yanayohusu haki, wajibu, uovu, maslahi na hisia za wananchi wa ngazi za msingi za jamii (grasroots) ambayo, licha ya unyeti wake kwa jamii hiyo na kwa taifa, hayapati nafasi katika vyombo vya habari, yanafunikwa na habari za kila siku za kisiasa na uchumi zinazogusa sehemu ndogo ya jamii

Usuli

- Kuyaibua masuala hayo kutasaidia kujenga uelewa na uwezo wa jamii kutambua juu ya haki na wajibu wao, kudadisi ama kuhoji maamuzi yasiyozingatia maslahi yao, kulinda rasilimali za taifa zilizo katika maeneo yao, kuchukua hatua dhidi ya uonevu, unyanyasaji, na ukiukwaji wa sheria na taratibu unaofanywa na wenye nafasi za kisiasa, kiuchumi, kihadhi, kidini n.k

Kwanini nishati uoto?

- Ni takribani miaka kumi sasa tangu harakati za kutumia nishati inayotokana na mimea zianze
- Sababu kubwa ni 3 kwanza ni tishio la kwisha kwa hifadhi ya mafuta ya asili ardhini, pili ni kupunguza uchafuzi wa mazingira hasa hewa na tatu , sababu za kiuchumi hasa kwa nchi za ulaya, kutafuta kujitegemea kwa mafuta badala ya kutegemea vyanzo vya mashariki ya kati.

Kwanini?

- Upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya kilimo cha mazao ya nishati mimea umeambatana na vitendo vya ukiukwaji mkubwa wa taratibu za kisheria na haki za binadamu kwa wamiliki wa ardhi hasa katika nchi za kiafrika.
- Baadhi ya vitendo ni pamoja na ukiukwaji wa makusudi wa taratibu za utwaaji na uhawilishaji wa ardhi hasa za vijiji ili kuwapa wawekezaji, rushwa, uondoaji wa wamiliki wa maeneo bila fidia au kwa fidia kidogo isiyo kamili, ya haki na ya wakati kama sheria inavyotaka
- Kushindwa kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kuishia kutoa maeneo yenye umuhimu wa kibaoanuai kwa wawekezaji (High Conservation Value areas)

Kwanini…

- Tangu mwaka 2007,HAKIARDHI imekuwa ikiyashughulikia masuala haya kwenye maeneo mbalimbali kwa kufanya tafiti, utetezi na ushawishi kwa watunga sera na sheria.
- Pia taasisi inaratibu mtandao wa mashirika yanayojishughulisha na masuala ya nishati uoto nchini maarufu kama Tanzania Bio energy forum –TABEF ambao umeweza kuibua na kufanya harakati kubwa sana za utetezi wa haki za wanyonge maeoneo mbalimbali. Wadau wakubwa wa mtandao huu ni pamoja na WWF, JET, ENVIROCARE, LEAT, TATEDO, TASGA, TNRF, MJUMITA, NEMC, na taasisi nyingine nyingi za wana mazingira nchini. Hata hivyo, juhudi hizi hazitoshi ndio maana kuna sababu ya kuongeza nguvu za wanahabari wachunguzi.

Kazi ya washindi wa tuzo

- Kufanya uchunguzi wa kina wa hali ya uwekezaji kwenye nishati mimea kwa lengo la kuibua masuala yaliyojificha lakini yanayoendelea kuwaathiri kwa namna mbalimbali wananchi na makundi mengine ya kijamii.
- Kubainisha fursa na manufaa mmbalimbali yanayoambatana na uwekezaji katika eneo hili ambayo hayajawekwa bayana katika uandishi na tafiti zilizokwisha fanyika
- Kuibuliwa kwa masuala hayo kutakuwa kichocheo cha mijadala na maamuzi sahihi katika ngazi mbalimbali za utoaji wa maamuzi kuanzia vijijini hadi kwa watunga sera na sheria ngazi ya taifa.

Mchakato wa kuwapata washindi …

- Tangazo lilitolewa katika vyombo vya habari (magazeti na mitandao ya kijamii) kualika waandishi kuwasilisha *concept notes (hoja za kiuchunguzi)* tarehe 27 Oktoba
- Jumla ya waandishi 6 waliwasilisha maandiko yao
- Waandishi 2 waliomba kuwasilisha lakini hawakuruhusiwa muda ulikuwa umepita
- Mchujo ulifanywa na kamati maalumu ya programu kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa

Mchakato …vigezo 6

- Aina ya chombo cha habari (print vs electronic)
- Kukidhi maelezo na mahitaji ya kwenye tangazo
- Uhalisia wa masuala yaliyoibuliwa na kuwasilishwa
- Uwiano kati ya taarifa na tathmini (maoni binafsi) ya mwandishi
- Marejeo
- Mpangilio wa andiko na uwezekano wa kukamilisha kazi ndani ya kipindi cha mwezi mmoja uliopangwa.

Matokeo ya mchujo

- Mwandishi mmoja aliandika makala nzuri sana lakini katika mtindo wa taarifa au kazi iliyokwisha fanyika –hakukidhi vigezo
- Waandishi watano walishindanishwa kwa vigezo vyote ndipo washindi 3 walipatikana. Wote ni washindi sawa, hakuna wa kwanza wala wa mwisho kwa vigezo vyetu.
- Washindi hao ambao napenda kuwatangaza rasmi bila kuorodhesha washindani wengine ni.:

WASHINDI

- GERALD KITABU – THE GUARDIAN
- AMIN ANTHON MGHENI – MLIMANI TV
- OBEID OTHMAN – MWANANCHI
- Napenda kuwapongeza washindani wote wa shindano hili na kuwapa moyo wale ambao hawakupata fursa wakati na kuwaalika wakati mwingine fursa kama hiii itakapojitokeza
- Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza sana washindi hawa na kuwatakia kazi njema za uandishi wa kiuchunguzi katika masuala ya nishati mimea kulingana na mawasilisho yao.

Mwisho

- Nawashukuruni nyote kwa kuja na kushuhudia hafla hii fupi ya utoaji wa tuzo kwa washindi wetu wa shindano la uandishi wa habari za kiuchunguzi kwenye masuala ya nishati uoto
  - ASANTENI SANA

myenzi@hakiardhi.org

16.11.2011